*Mwanza, 02 Desemba, 2025*

# TAARIFA KWA UMMA

## MAAMUZI YA TUME YA VYUO VIKUU TANZANIA KUSITISHA KIBALI CHA UDAHILI NA USAJILI WA WANAFUNZI WA MWAKA WA KWANZA WA SHAHADA YA UDAKTARI WA BINADAMU KATIKA CHUO KIKUU MWANZA (MzU) KWA MWAKA WA MASOMO 2025/2026

### 1.0 UTANGULIZI

Itakumbukwa kuwa, kuanzia tarehe 15 Julai hadi 20 Oktoba, 2025 Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) iliratibu maombi ya udahili kwa wanafunzi wa Shahada ya Kwanza, mwaka wa masomo 2025/2026 kwa vyuo vyote vya elimu ya juu nchini. Maombi hayo ya udahili yalikuwa yakitumwa moja kwa moja vyuoni, na hivyo vyuo kuendelea na utaratibu wa udahili kupitia Seneti zao kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za udahili na uendeshaji wa elimu ya chuo kikuu nchini.

Baada ya kukamilika kwa zoezi la udahili, TCU ilifanya ukaguzi wa awali kwa lengo la kuhakiki uzingatiaji wa vigezo vya udahili, ikiwemo idadi ya wanafunzi kwa programu za masomo, sifa za kitaaluma na vigezo vingine stahiki vilivyoidhinishwa na Tume pamoja na bodi/mabaraza ya usajili wa wataalamu.

Ukaguzi umebaini kuwepo kwa ukiukwaji mkubwa wa taratibu za udahili na usajili wa wanafunzi wa Shahada ya Kwanza katika Chuo Kikuu Mwanza (MzU) ambapo, chuo kimedahili na kusajili idadi kubwa ya wanafunzi mara kumi ya idadi iliyoidhinishwa na mamlaka ya urekebu (TCU) kwa Shahada ya Udaktari wa Binadamu kwa mwaka wa masomo 2025/2026. Idadi husika ni kubwa kuliko uwezo wa chuo kimiundombinu ya kujifunzia na kufundishia ikiwamo idadi ya walimu waliopo.



Jengo la SUMA JKT, S.L.P 2600, 1 Mtaa wa JKT, 4110 Tambukareli, Dodoma
Jengo la Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, S.L.P 6562, 7 Mtaa wa Magogoni, 11479 Dar es Salaam,
Simu: +255 22 2113694, 2113691, Nukushi: +255 2113692, Barua Pepe: es@tcu.go.tz, Tovuti: www.tcu.go.tz

## 2.0 MAAMUZI YA TUME KWA CHUO KIKUU MWANZA

Kutokana na ukiukwaji mkubwa wa taratibu za udahili na maelekezo ya Tume, na kwa kuzingatia umuhimu wa kuwa na wahitimu wenye kukidhi viwango vya ubora wa elimu kitaifa, Tume katika kikao chake maalum cha 127 kilichofanyika tarehe 28 Novemba 2025, imefanya maamuzi yafuatayo:

### 2.1 Kusitisha Kibali cha Udahili na Usajili wa Wanafunzi wa Mwaka wa Kwanza kwa Mwaka wa Masomo 2025/2026

Tume imesitisha kibali cha udahili na usajili wa **wanafunzi wa mwaka wa kwanza** wa Shahada ya Udaktari wa Binadamu kwa Chuo Kikuu Mwanza (MzU) katika mwaka wa masomo 2025/2026. Usitishwaji huu unatokana na chuo husika kushindwa kuzingatia maelekezo ya Tume, kwa kudahili na kusajili idadi kubwa ya wanafunzi kuliko ile iliyoidhinishwa na kuchapishwa kwenye kitabu cha Mwongozo wa Udahili kwa mwaka wa masomo 2025/2026. Aidha, Chuo Kikuu Mwanza kilishindwa kufanya marekebisho ya idadi hiyo licha ya kupewa maelekezo ya kufanya hivyo.

Chuo hicho kitaendelea kutoa mafunzo kwa wanafunzi wengine wanaoendelea na masomo.

### 2.2 Kutoa Kibali kwa Wanafunzi Wote wa Mwaka wa Kwanza Kuhamia Vyuo Vingine

Tume imetoa kibali cha kuwapa fursa wanafunzi wa mwaka wa kwanza waliodahiliwa, kusajiliwa na kuripoti chuoni hapo, kuomba kuhamia vyuo vingine vilivyoruhusiwa kudahili wanafunzi katika programu ya Udaktari wa Binadamu au programu nyingine wanazozitaka, kwa mwaka wa masomo 2025/2026 au miaka inayofuata.

### 2.3 Chuo Kikuu Mwanza Kiwataarifu Wanafunzi na Kuwasaidia Kukamilisha taratibu za Uhamisho

Chuo Kikuu Mwanza (MzU) kimeelekezwa kuwataarifu wanafunzi husika kuwa chuo hakitatoa masomo kwa mwaka wa kwanza katika mwaka wa masomo 2025/2026 kutokana na kutokidhi taratibu za uendeshaji wa elimu ya chuo kikuu. Hivyo, chuo kinapaswa kuwasaidia wanafunzi hao kutafuta uhamisho kwenda vyuo vikuu vingine ambavyo viko tayari na vina uwezo wa kuwapokea wanafunzi husika.



Jengo la SUMA JKT, S.L.P 2600, 1 Mtaa wa JKT, 4110 Tambukareli, Dodoma
Jengo la Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, S.L.P 6562, 7 Mtaa wa Magogoni, 11479 Dar es Salaam,
Simu: +255 22 2113694, 2113691, Nukushi: +255 2113692, Barua Pepe: es@tcu.go.tz, Tovuti: www.tcu.go.tz

Tume inawaasa wanafunzi walioathirika na mabadiliko haya kuwa watulivu kwa kuwa suala hili linashughulikiwa kwa kuzingatia maslahi mapana ya wanafunzi na jamii kwa ujumla. Tume kwa kushirikiana na Chuo Kikuu Mwanza, pamoja na vyuo vitakavyowapokea wanafunzi husika, itahakikisha kuwa mchakato wa uhamisho unatekelezwa kwa haraka na ufanisi.

### 2.4 Kuundwa kwa Kamati/Timu ya Wataalamu Kuchunguza Maswala ya Kitaaluma katika Chuo Kikuu Mwanza

Ili Tume iweze kuchukua hatua stahiki, ikiwamo kuhakikisha Chuo Kikuu Mwanza kinazingatia sheria, kanuni na taratibu za uendeshaji wa elimu ya chuo kikuu, Tume imeunda kamati/timu ya wataalamu kuchunguza mchakato mzima wa masuala ya kitaaluma chuoni hapo. Kamati hiyo itaanza kazi mara tu baada ya zoezi la uhamisho kukamilika.

## 3.0 HITIMISHO

Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania inaendelea kutekeleza jukumu lake la uthibiti ubora wa elimu ya chuo kikuu kwa vyuo vikuu vyote nchini. Aidha, Tume itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali wa elimu ya chuo kikuu kwa lengo la kuhakikisha kuwa elimu inayotolewa inakidhi vigezo vya ubora kitaifa, kikanda na kimataifa.

Tume itaendelea kuchukua hatua stahiki katika kuhakikisha vyuo vikuu vinazingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo iliyopo ya uendeshaji wa elimu ya chuo kikuu nchini.

Imetolewa na:



Prof. Charles D. Kihampa

**KATIBU MTENDAJI**

**TUME YA VYUO VIKUU TANZANIA**



Jengo la SUMA JKT, S.L.P 2600, 1 Mtaa wa JKT, 4110 Tambukareli, Dodoma
Jengo la Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, S.L.P 6562, 7 Mtaa wa Magogoni, 11479 Dar es Salaam,
Simu: +255 22 2113694, 2113691, Nukushi: +255 2113692, Barua Pepe: es@tcu.go.tz, Tovuti: www.tcu.go.tz